



OFFICE OF THE MAYOR

MAYOR: Lauren McLean

MWONGOZO WA RASILIMALI ZA COVID-10 (VIRUSI VYA KORONA) WA MJI WA BOISE

Ujumbe kutoka Diwani Lauren McLean

Najua kwamba janga la COVID-19 limekuwa ligumu kwa jamii yetu. Maisha yetu yamepinduka. Hatuna uhakika kwa yatayo tokea, jinsi maisha yetu yatavyo badiliki kutoka siku moja hadi nyingine na ni changamoto gani tutakazo pambana nazo. Tafadhali jua kwamba sisi hapa kwenye mji wa Boise tuna hakikisha afya na usalama wa jamii yetu kwa uzito.

Ni muhimu kila mtu atimize upande wake ili tupunguze mwendo wa kuenea wa virusi ili hospitali zetu zisilemewe na wakaaji walio hatarini wa hifadhiwe.

Nina uhakika kwamba tutajitokeza kwa nguvu na tupate nafuu pamoja kama jamii. Tuko pamoja, Boise.

SASISHO ZA CDC ZA COVID-19: <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/index.html>

SASISHO ZA JIMBO LA IDAHO <https://coronavirus.idaho.gov/>

SASISHO ZA MJI WA BOISE ZA COVID-19: www.cityofboise.org/covid19

SASISHO ZA JIMBO LA IDAHO

- **Amri ya jimbo nzima kubakia nyumbani iliyo tolewa na Gavana Little**
- Amri hii iliyo tolewa mwezi wa Machi tarehe 25, ina ufanisi wa siku 21. Kila mkaaji wa Idaho lazima akae nyumbani isipo kuwa kama anafanya huduma muhimu (tazama orodha ya huduma muhimu) au kama wana hitaji huduma muhimu.
 - Nenda: www.coronavirus.idaho.gov kwa maelezo zaidi, pamoja na huduma muhimu.
 - Wasiliana na wilaya ya afya ya umma iliyo karibu. Njia za kuasiliana nao yaweza patikana hapa: <https://coronavirus.idaho.gov/contact/>

SASISHO ZA MJI WA BOISE

Vituo vifuatavyo vya mji wa Boise vimefungua hadharani:

- Ukumbi wa jiji

- Ukumbi wa Jiji wa magharibi
- Mkataba za umma za Boise, pamoja na Maktaba kuu na kila tawi la maktaba
- Fort Boise pamoja na kituo cha wazee cha Dick Eardley (Kipindi cha kupeleka chakula nyumbani kitatimizwa kando ya barabara)
- Vituo vya jamii vya shuleni
- Idaho IceWorld
- Bustani ya wanyama ya Boise (Zoo Boise)
- Uwanja wa gofu wa Quail Hollow
- Uwanja wa gofu wa Warm Springs
- Tengamaji ya Boise (Boise WaterShed)
- Nyumba ya James Castle
- Vyoo vyote vya bustani (Vyoo visivyo vya kudumu vita wekwa kwenye sehemu za kutumiwa sana)
- Vyoo vyote kwenye utambaazi
- Bustani zote za ku-skate
- Bustani zote zilizo na nyuzio za mbwa wasiofungwa (masaa ya sehemu za bila kufungwa na bustani za bila kufungwa hayajathiriwa)
- Bustani ya baiskeli ya J.A. na Kathryn Albertson Foundation
- Bustani ya J.A. na Kathryn Albertson Family Foundation ya Whitewater
- Bustani zote za watoto kuchezea zimefungwa

Huduma zinazo tolewa kibinafsi zitatolewa kupitia kwenye mtandao (ikiwezekana), kwa simu, kupitia barua au kuhairishwa hadi huduma za umma zitakazo rejeshwa.

Pia mabadiliko ya huduma zifuatazo ziko tayari:

- Vipindi vya umma vya mji mzima pamoja na vya kufikia umma vime hairishwa hadi taarifa zaidi.
- Sehemu ya kubeba mbolea ya Idaho Botanical Gardens na Joplin Road zime fungua.
- Sehemu ya kupeleka glasi za kuchakata imefungwa.
- Mkusanyiko wa uchafu wa uhatari nyumbani umesimamishwa.
- Mkusanyiko wa vitu vikubwa imesimamishwa isipo kuwa kama kuliwa na mpango tayari.
- Sehemu za kurudisha vitabi kwenye maktaba zimefungwa. Tafadhali bakia na vitu kyakoiusipokuwa kama umepata mawasiliano mengine. Tarehe ya kurejesha imeongezwa hadi mwezi wa Juni tarehe 1, mwaka wa 2020.
- Utelekezaji wa maegesa na kutimiza kodi zimesimamishwa kwa mda huu wa amri ya gavana ya kubakia nyumbani (isipokuwa ukaguaji wa utunzaji wa watoto)
- Utelekezaji wa wanyama umesimamishwa kwa mda wa amri ya gavana ya kubakia nyumbani.
- Ukaguzi wa majenzi na moto zita endelea kwa mijengo lakini kwa kikomo na upungufu wa wafanyi kazi. Miongozo ya CDC lazima itimizwe wakati wa ukaguzi ili afya na usalama za wafanyi kazi zihifadhiwe.



Ushirika kati ya wilaya ya shule ya Boise pamoja na Bustani na Maburudisho ya mji wa Boise zimetoa vituo vya mchana mzima bila malipo kwenye shule ya Whittier Elementary na Morley Nelson Elementary.

- Walisiana na: Emily Kovarik – ekovarik@cityofboise.org

SASISHO ZA WILAYA YA SHULE

- Wilaya ya shule ya Boise pamoja na ya West Ada zime fungwa hadi mwezi wa Aprili tarehe 20 mwaka wa 2020.
- Wilaya ya shule ya Boise inawapa watoto (wa umri wa mwaka 1 hadi 18) chakula cha kunyakua-na-kwenda bila malipo. Watoto wanaeza chukua chakula kati ya saa tatu na saa nne za asubuhi. Hakuna haja ya kitambulisho au ushahidi wa kujiandikisha shuleni lakini lazima mtoto awe hapo. Sehemu zilizo na chakula bila malipo ni:
 - Morley Nelson Elementary (7701 W Northview St)
 - Whitney Elementary (1609 S Owyhee St)
 - Grace Jordan Elementary (6411 W Fairfield Ave)
 - Whittier Elementary (301 N 29th St)
- Wilaya ya shule ya West Ada inawapa watoto wa umri wa mwaka 1 hadi 18 chakula cha kifungua kinyua na cha mchana zikiwa pamoja kutoka saa tano za asubuhi hadi saa saba za mchana bila malipo. Chakula kinapeanwa kwenye njia za basi za shule na kwenye sehemu iliyo teuliwa hapo mbele ya shule. Sehemu hizo ni pamoja na:
 - Meridian Middle
 - Lewis and Clark Middle
 - Frontier Elementary
 - Chief Joseph Elementary
 - Spalding Elementary
 - Renaissance High School
 - Ustick Elementary
 - Desert Sage Elementary
 - Peregrine Elementary
 - McMillan Elementary
 - Barbara Morgan
 - Mary McPherson
 - Chaparral Elementary
- Idara ya Bustani na Maburudisho ya mji ya Boise imetoa vituo vya mchana mzima bila malipo kwenye shule za Whittier Elementary na Morley Nelson Elementary.



SASISHO ZA HOSPITALI

- **Hospitali ya St. Luke's**
 - Sehemu za nje za kufanya kipimo cha COVID-19 ukiwa kwenye gari ziko kwenye hospitali zao za Boise na Meridian.
 - Nambari ya simu ya moja kwa moja ya kuelewa ukali wa ugonjwa wa COVID-19 ni (208) 381-9500
 - Mtandao wa rasilimali: <https://www.stlukesonline.org/blogs/st-lukes/notes-and-announcements/2020/mar/st-lukes-covid-19-coronavirus-announcement> [nam01.safelinks.protection.outlook.com]
- **Hospitali ya Saint Alphonsus**
 - Sehemu ya nje ya kuchunguza ugonjwa wa COVID-19 ukiwa kwenye gari iko kwenye Meridian Health Plaza, (3025 W Cherry Lane)
 - Nambari ya simu ya moja kwa moja ya COVID-19 ni (208) 302-2683
 - Mtandao wa rasilimali: <https://www.saintalphonsus.org/coronavirus/>
- **Saltzer Medical**
 - Uchunguzi wa kando ya barabara upo kwenye sehemu ya Nampa
 - Nambari ya simu ya moja kwa moja ya COVID-19 ni (208) 463-3000 ext.7
 - Mtandao wa rasilimali: <https://saltzerhealth.com/coronavirus/>

DALILI YA MAONYO

Ukipata dalili za dharura za COVID-19, pata matibabu hapo hapo. Dalili hizi ni pamoja na:

- Uguma wa kupumua au upungufu wa pumzi
- Maumivu yanayo dumu au shinikizo kwenye kifua
- Machafuko mapya au kutoweza kuamka
- Midomo au uso ulio na rangi ya buluu

* Orodha hii sio kamilifu. Tafadhali pata ushauri wa dkatari wako ukiwa na dalili zingine kali au zinazo kutia mashaka.



PRIMARY HEALTH

Ukidhani kwamba umefunuliwa kwa COVID-19 au unahitaji kupimwa kwa uwezekano wa maambukizi ya COVID-19, tafadhali pigia simu mmoja ya kliniki za Primary Health za kupumua iliupate miada ya siku hiyo hiyo na ubaki kwenye gari lako ukiwasili.

Primary Health, Garden City (5601 W. Chinden Blvd.): 208-809-2865

Primary Health, Meridian Crossroads (3280 E. Lanark Dr.): 208-895-8670

Primary Health, Nampa (700 Caldwell Blvd): 208-466-6567

Utafsiri upo kupitia Primary Health